



Parti CNDD-FDD  
Conseil National pour la Défense  
de la Démocratie - Forces pour la  
Défense de la Démocratie.

Umugambwe CNDD-FDD  
Inama y'abanyagihugu baharanira  
Demokarasi.

## **TANGAZO LA CHAMA CHA CNDD FDD KUHUSU FIKRA YA KUANZISHWA KWA BARAZA LA KITAIFA AJILI YA KUHESHIMISHA MKATABA WA AMANI WA ARUSHA NA KATIBA NCHINI BURUNDI.**

Chama cha CNDD FDD kinacho teteya uheshimishaji wa sheria (Épris du Respect de la Loi) , vyama vya kisiasa vya upinzani na mashirika ya kiraia waliyo ungana kwa pamoja kupinga muhula wa tatu wa Rais Pierre Nkurunziza , wametangaza hapo July 15 iliyopita, kuwepo fikra ya kuanzishwa kwa Baraza la Kitaifa ajili ya kuheshimisha Mkataba wa Amani wa Arusha na Katiba nchini Burundi. Kufuatia azma hio, chama cha CNDD FDD kinacho teteya uheshimishaji wa sheria kinatangazia jamii ya kitaifa na kimataifa haya yafuatayo :

1. Chama hiki daima kinaheshimu sera zake anzilishi na azma yake ikiwa ni pamoja na kutetea na kudumishwa kwa utawala unao heshimu haki na wakati huo huo kupiga vita ubaguzi wa aina yoyote dhidi ya raia wake.
2. Chama kinasikitishwa na hali mbaya mno inao endelea nchini Burundi katika sekta za kijamii, kisiasa na kiuchumi, na ambayo inatokana na utawala mbovu na hali duni ya usalama inayo tanda nchi nzima.
3. Chama cha CNDD FDD kinacho tetea uheshimishaji wa sheria nchini Burundi kina uwasiwasi mkubwa kuhusu ukaidi wa Pierre Nkurunziza kusalia madarakani kwa kuvunja Katiba ya Nchi, Mkataba wa Amani na maridhiano wa Arusha na Sheria zote zinazo baini Mfumo wa siasa uliyo mfikisha kwenye uongozi wa nchi.
4. kufuatia msingi wa kidemokrasia unao kijenga chama cha CNDD FDD kinacho tetea uheshimishaji wa sheria, Chama hiki kinatangaza bayana kuunga mkono juhudi za kuanzishwa kwa Baraza la Kitaifa ajili ya kuheshimisha Mkataba wa Arusha na Katiba nchini Burundi. Aidha chama hiki kimeelezeya utashi wake kushirikiana na makundi yote hadi kupatikana ufumbuzi kwa amani wa mzozo wa sasa nchini Burundi, na kudumishwa amani na usalama kwa raia wote, utengamano na kuanzishwa utawala bora nchini Burundi.

5. Chama cha CNDD FDD kinacho teteya uheshimishaji wa sheria kinaitoleya mwito jamii ya kimataifa kuwapa misaada zaidi ya kibinaadam wakimbizi warundi waliyoko mataifa jirani kufuatiya mgogoro wa sasa na kutoa mwito wa michango zaidi ya kifedha kukabiluana na wimbi kubwa la wakimbizi wanao ongezeka.
6. Chama cha CNDD FDD kinaitumiya fursa hii kuomboleza familia zilizo athiriwa na wakati huo huo kupongeza mchango wa raia waliyo jitoa muhanga kudai kuheshimiwa sheria na kutetea hadhi ya warundi kwa ujumla katika kipindi chote cha maandamano ya amani ya umma. Mwenyezi Mungu awalaze pema peponi.
7. Chama cha CNDD FDD kinacho teteya uheshimishaji wa sheria kinawapongeza wafadhili na marafiki wa Burundi kwa mchango wao wa kuanzishwa kwa jitihada za sasa ambapo majukumu lengwa ni kutafutiya ufumbuzi wa kudumu changamoto mbalimbali kuhusu amani na usalama , msingi utakao pelekeya pelekeya kuanzishwa utawala bora nchini Burundi.
8. Kikao kinacho tazamiwa kuanzishwa rasmi Baraza la Kitaifa ajili ya kuheshimisha Mkataba wa Amani wa Arusha na Katiba nchini Burundi huenda kikafanyika barani humu mjini Addis Abeba kuliko makao makuu ya Umoja wa Afrika, ama mjini Pretoria kutokana na jukumu la Afrika ya kusini katika kufikiya hapo nyuma kwenye mazungumzo ya kusitisha mapigano katika ya pande zilizo kuwa zikihasimiana nchini Burundi. Imeandikwa Bujumbura, July18/2015. Rais wa chama cha CNDD FDD kinacho teteya uheshimishaji wa sheria.

Hon. Hadj **Hussein Radjabu**